UHARAMISHO WA U W O N G O

KATIKA UISLAMU

(Juzuu ya pili)

Kimekusanywa na kutarjumiwa na
Amiraly M.H Datoo
BUKOBA - TANZANIA

UHARAMISHO WA UWONGO JUZUU YA PILI

© Haki ya kumiliki imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN # 9987 – 665 – 13 – 6

Kimekusanywa na kutarjumiwa na:
Amiraly M. Datoo
S.L. P. 838
Bukoba – Tanzania.

Toleo la kwanza: Desemba 2002
Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION
S. L. P. 1017
Simu: 255-22-2110640
Fax: 255-22-2126757
Dar-es-Salaam.

Email: *alitrah@daiichicorp.com*

Website: *www.alitrah.org*

Y A L I Y O M O

Utangulizi.....6
Uharamisho wa Kusema Uwongo.....7
Malaikahutuma laana..... 8
Ayah za Qur'an Tukufu zinazo zungumzia uwongo.....9
Madhambi ya uwongo kugawanywa katika sura arobaini.....9
Uwongo ni Ufasiki.....9
Kauli 'dhur' Imaanishavyo.....10
Msema uwongo hawezi kuwa Mumiini.....10
Uwongo ni dhambi.....10
Mwongo ni maluuni.....10
Uso wa mwongo huwa mweusi.....10
Dhambi ya mwongo inazidi dhambi ya mlevi.....12
Mdomo wa mwongo hunuka harufu mbaya..... ..12
Malaika pia wanachukizwa.....12
Uwongo ni sababu za kufr..... 12
Mwongo hunuka vibaya.....13
Malaika humlaani mwongo..... .13
Uwongo huangamiza imani.....13
Uwongo unamkosesha mtu asiweze kuionja Imani..... ...13
Uwongo unaleta chuki na uadui.....13
Uwongo humwangusha mtu katika macho ya heshima na staha.....13
Uwongo ni ufunguo wa mabaya..... 14
Uwongo ni ufasiki.....14
Malaika elfu sabini wanamlaani mwongo.....14
Uwongo ni alama ya unafiki.....14
Ushauri wa mwongo kisheria haupendekezwi..... 14
Uwongo ni ugonjwa mbaya kabisa wa kiroho.....14
Uwongo ni urembo wa mkono wa Shetani..... 14
Katika anachojichumia mwanaadamu uwongo ndio kitu kiovu.....15
Uwongo unawaingiza Motoni.....15
Mwongo huugusa ugonjwa wa kusahau.....15
Msema uwongo huadhibiwa vikali..... 16
Mwongo hukosa sala za usiku wa manane (salatul Layl).....16

Uwongo ndiyo sababu ya kukosa hidaya na kujipatia upotofu.....17
Uwongo huondoa ubinadamu.....17
Uwongo ni uovu na uchafu mkubwa.....17
Uwongo upo mbali na imani bali tuseme kuwa ni kinyume
cha imani.....17
Mwongo ndiye mwenye madhambi mengi kuliko wote.....17
Mwongo hujiteketeza kwa uwongo wake.....18
Mwongo hastahiki kuwa ndugu na rafiki wa watu.....18
Allah s.w.t hawaongozi wafujaji na waongo.....18
Mwongo huonekana kuwa ni binadamu, lakini sivyo.....18
Daraja mbali mbali za uwongo.....19
Kuwazulia uwongo Allah s.w.t Mtume s.a.w. na Maimamu a.s.....19
Uwongo hata ukiwaje.....20
Kazi maalumu kwa watu maalumu.....20
Mfano wa kumzulia uwongo Allah s.w.t.....21
Kuzua uwongo dhidi ya Mtume Muhammad s.a.w.
na Maimamu a.s.....21
Riwaya zitolewe pamoja na mnyororo wa mapokezi.....22
Kuelezea Madhumuni ya Riwaya.....23
Kujiepusha na viapo viongo na ushahidi wa kiwongo.....24
Athari mbaya za uwongo 24
Uwongo kwa kusema katika kicheko na mzaha.....24
Kujiepusha na uwongo kwa kikamilifu.....25
Kurejea si Uwongo.....27
Tusidhanie kila uwongo kuwa ni 'mdogo tu'.....27
Uwongo wa ndoto.....28
Uwongo katika kutoa mifano.....29
Al-Imamu Husayn ibn 'Ali ibn Abi Talib a.s atoa mfano.....29
Kusikiliza uwongo pia ni haramu.....30
Je 'Tawriyyah' ni nini.....31
Hukumu za 'Tawriyyah'.....32
Mahali ambapo kusema uwongo umeruhusiwa 33
Kiapo cha uwongo kwa ajili ya kuwanusuru Waislamu.....33
Hasara ya mali na uwongo.....34
Afanye Tawriyyah kiasi awezacho..... 35
Kuwasuluhisha Mumini wawili kwa kutumia uwongo.....35
Ujumbe Mkali.....36

Usuluhisho miongoni mwa watu.....…..36
Maji ya Kur na Umoja wa Moyo.....…37
Uwongo Vitani..... .39
Kumuahidi Mke wako.....…..39
Hofu ya adhabu na matendo mema.....…41
Kile kilicho mdomoni ndicho hicho hicho kiwe moyoni.....…42
Kufanya ‘Ibada na uwongo.....…43
Uwongo katika Dua.....…43
Kukiri kuwakubali ‘Aimma a.s kusema uwongo.....….43
Je anasema kweli.....…44
Kuwaambia uwongo Maimamu (a.s).....…44
Sasa je tuombeje Dua.....….45
Kila mtu ana daraja lake.....…46
Yakini na Uhalifu.....….47

UTANGULIZI

Namshukuru Allah swt pamoja Mtume Muhammad s.a.w.w. na Maimamu a.s. kwa kunijaalia kukitayarisha kitabu hiki.

Ni matumaini yangu kuwa maudhui haya yatatunufaisha na kutuelimisha sisi wote ili tuweze kujiepusha sisi wenyewe natusiwachochee wengine wakatumbukia katika ugonjwa huu wa kusema uwongo.

Vitabu vingine pia vimetayarishwa katika mfululizo huu wa kuyarekebisha na kuyatokomeza mabaya katika jamii yetu kama :

1. Uharamisho wa Kamari,
2. Uharamisho wa Ulevi
3. Uharamisho wa Riba
4. Uharamisho wa Uwongo (juzuu ya kwanza)
5. Uharamisho wa Uwongo (juzuu ya pili)
6. Ulawiti –Dhambi Kuu
7. Uharamisho wa Zinaa
8. Usamehevu katika Uislamu.

Ni matumaini yangu kwamba mawaidha na nasiha zilizomo katika vitabu hivi vitatusaidia katika kuishi maisha mema na kuachana na mabaya.

Wabillahi Tawfiq,
Nduguyo katika Uislamu,

Amiraly M.H.Datoo *2nd May 2001*
P.O.Box 838
BUKOBA
Tanzania (E.Africa)
e-mail : *datooam@hotmail.com*

Na unaweza kupata hazina ya elimu katika lugha ya Kiswahili katika mtandao wa kompyuta kwa anwani : *http://www.al-islam.org*/kiswahili.

Uharamisho wa Kusema Uwoango [1]

Allah swt anatuambia katika Qur'an Tukufu ***Surah An-Nahl,16, Ayah ya 105 :***

'Wanaozua uwongo hawana imani'

Vile vile Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema :

"*Mtu mwovu kabisa ni yule ambaye ni msema uwongo."*

Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema :

"Allah swt humlaani mwongo hata kama atasema ukweli"

Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema:

"Jitahadharisheni, Mimi ninawaambieni dhambi Kubwa kabisa katika dhambi kubwa :

- *Kumshirikisha Allah pamoja na mtu mwingine*
- *Kumuambia mzazi 'Aqh*
- ***Na kusema uwongo***

Al-Imam 'Ali ibn Abi Talib a.s. amesema :
"Ugonjwa wa kusema uwongo ndio ugonjwa mbaya kabisa."

Vile vile Imam Hasan al-'Askari amesema katika *Mustadrad al-Wasa'il,Kitabu Hajj, mlango wa 12*:

"Maovu yote yamefungwa katika chumba kimoja kwa kufuli, na uwongo ndio ufunguo wake."

Amesema al-Imam Musa ibn Ja'afar a.s. :

"Mtu mwenye busara kamwe hawezi kusema uwongo hata kwa matamanio yake mwenyewe."

Al-Imam 'Ali ibn Abi Talib a.s. amesema :

“Itakuwa vyema kwa Waislamu iwapo hawatafanya urafiki na udugu pamoja na Mwongo.”

Amesema al-Imam Muhammad al-Baqir a.s. katika *Al-Kafi, j.2*:

“Uwongo unateketeza misingi ya Imani.”

Malaika hutuma laana

Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema katika *Al-Mustadrak al-Wasail* :

“Mumini anaposema uwongo bila ya shida yeyote,basi Malaika elfu sabini humlaani !!”
“Na hutoka harufu mbaya kabisa kutoka moyoni mwake, harufu hiyo hufika hadi ‘arsh .”

“Na Allah swt humwandikia kwa dhambi hiyo moja, dhambi sabini za zinaa na zinaa yenyewe si zinaa ya kawaida bali zinaa pamoja na mama yake .”

Bila shaka hakuna dhambi iliyo kubwa kama dhambi hii ya kusema uwongo. Hivyo inamaanisha kwamba madhara ya kusema uwongo yanazidi mno madhara ya zinaa. Baadhi ya uwongo huwagombanisha vikali makabila mawili na kuzusha vita miongoni mwao. Kutokana na uwongo maisha na heshima na mali ya watu wengi hupotea na kuteketea. Upo uwongo na uzushi mwingi ambao anatupiwa Allah swt, Mtume Muhammad s.a.w.w. na Maimamu a.s.
Ni dhahiri kuwa madhambi kama haya ya kusema na kusingizia uwongo ni matendo ya kudhalilisha na yenye kustahiki adhabu kali kutoka kwa Allah swt.

Tumeyasikia na kujionea kwamba kwa sababu ya kutoa ushahidi wa uwongo, watu wamenyongwa na majumba kuteketezwa ndiyo maana tunapata katika riwaya moja isemayo : ‘Uwongo ni mbaya zaidi kuliko ulevi.’

Ayah za Qur'an Tukufu zinazo zungumzia Uwongo

Allah swt anatuambia katika Qur'an Tukufu **Surah An-Nahl,16, Ayah ya 105 :** *'Wanaozua uwongo hawana imani'*

Vile vile Allah swt anatuambia katika **Surah Az-Zumar ,39, Ayah ya 3**…"Hakika Allah hamuongoi aliye mwongo, kafiri."

Kwa mujibu wa Ayah za Qur'an Tukufu tunaambiwa kuwa mwongo ni mwenye kustahili adhabu ya Allah swt. Na Allah swt huwa daima amemghadhibikia. Kama vile tuonavyo katika Ayah zifuatazo :

> ***Surah Aali-Imran, 3, Ayah ya 61****…." Tutake laana ya Allah swt iwashukie waongo."*
>
> ***Surah An-Nuur ,24 , Ayah ya 7 :****"… Laana ya Allah iwe juu yake iwapo ni miongoni mwa waongo."*

Madhambi ya uwongo kugawanywa katika sura arobaini.

Marehemu Al-Haj Nuuri (a.r.) ametayarisha kazi moja nzuri kwa kugawa madhambi na madhara yake katika sura arobaini kwa mukhtasari ambao ninapenda kuwaletea:

Uwongo ni Ufasiki

Allah swt anatuambia katika Qur'an Tukufu ***Surah Baqarah, 2, Ayah ya 197*** kuwa : 'Na katika Hajj hairuhusiwi maneno machafu wala ufusuka.' Katika Ayah hii takatifu neno 'fisq' inamaanisha **uwongo** kwa mfano katika ***Surah Al-Hujurat ,49, Ayah ya 6*** tunaona kuwa uwongo unaitwa kuwa ni 'ufasiki'. Ayah yenyewe inasema : 'Enyi mlioamini ! Iwapo mtaijiwa na mwongo na habari yoyote basi msikubalie tu bali mufanye upelelezi…..'

Katika Ayah hii Walid alitambulishwa kwamba ni mwongo..

Kauli ‘dhur’ inamaanishavyo

Tumepewa hukumu ya kujiepusha na kuabudu sanamu na kutosema uwongo na inasemwa kuwa : ‘*Basi mjiepusheni na uchafu (wa mfano wa sanamu) na jiepusheni na maneno ya uwongo.’* **Surah Al-Haj, 22, Ayah ya 30** Hapa *qauli dhur* au *laghwu* inamaanisha **uwongo.**

Msema uwongo hawezi kuwa Mumiini

Kwa mujibu wa Ayah ya Sura ya An-Nahl, 16, Ayah ya 105, imethibitika kuwa msema uwongo hawezi kuwa Mumin na mtu aliye Mumin kamwe hawezi kusema uwongo. Ni dhahiri kuwa kutokuwa na imani juu ya ‘dalili’ za Allah swt basi mtu hawezi kuwa Mumin.

Uwongo ni dhambi

Katika riwaya dhambi inaitwa *Ithm* au *Dhamb.* Kwa mfano amesema al-Imam Muhammad al-Baqir a.s. : “*Uwongo wowote ni ithm na dhamb.”*

Mwongo ni maluuni

Mwongo huwa ni mustahiki wa laana na ghadhabu za Allah swt na mfano wa kauli isemwayo katika ***Surah An-Nuur, 24 Ayah ya 7*** *isemayo : ‘‘... Laana ya Allah iwe juu yake iwapo ni miongoni mwa waongo.’*

Uso wa mwongo huwa mweusi.

Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema katika *Mustadrak al-Wasail* kuwa *“Jiepusheni na uwongo kwani uwongo huufanya uso kuwa mweusi.”*

Katika kitabu kiitwacho *Habibu Siyar* imeandikwa kisa kifuatacho

“Wanahistoria wanaandika; “Kulikuwapo na uhusiano mzuri baina ya Sultan Boyghora, Mfalme wa Khurasaan na Zabulistan, na Sultan Ya’aqub, Mfalme wa Iraq na Azarbaijan na walikuwa wakiwasiliana daima kati yao.

Mfalme wa Iran aliamua kumtumia zawadi ya vito vya thamani kwa Sultan Ya’aqub. Wakati zawadi zilipokuwa tayari, yeye aliamrisha kuongezewa maandiko ya Jami’ katika zawadi hizo ambayo yalikuwa mashuhuri siku hizo.

Mkutubi, Mulla Abdul Karim, alifanya kosa wakati wa kufunga kifurushi cha kitabu cha Jami’ na badala yake alikituma kitabu kilicho zungumzia ushindi wa Makkah ambacho kilikuwa sawa na jalada kwa ukubwa.

Mheshimiwa katika Baraza la Mfalme, Amir Husain Abiwardi, ndiye aliyepewa jukumu la kufikisha zawadi hizo hadi kwa Sultan Ya’aqub. Abiwardi, naye pia bila ya kukagua zawadi zilizokuwa ndani ya kifurushi, aliondoka na kuziangalia zawadi hizo.

Wakati Amir Husain alipowasili Tabriz Sultan Ya’aqub alimpokea kwa wema na kumkirimu na kusema : “Lazima utakuwa umechoka kwa safari iliyokuwa ndefu.” Kama vile Amir Husain alivyokuwa akijua kuwa Sultan aliipenda sana Jami’ , alisema : “Mimi nilikuwa ninaye rafiki mwema safarini hivyo sijisikii uchovu wa safari.”

Sultan alimuuliza kuhusu rafiki huyo, naye alimjibu : “Jami’ kazi za ushairi.” Sultan alifurahishwa mno kwa kusikia hivyo na alimtuma akilete kitabu hicho haraka iwezekanavyo, na wakati walipokifungua kifurushi waliona kwa masikitiko makubwa kuwa si kitabu chenyewe bali kilikuwa ni kitabu juu ya ukombozi wa Makkah.

Amir Husain alishikwa na aibu kubwa kwa kusema uwongo, lakini alikuwa amekwisha chelewa kwa ajili ya kufanya marekebisho. Mwanadiplomasia huyo mkongwe alikuwa ameadhirika na kudhalilika katika nchi zote mbili na kupoteza heshima yake.”

Dhambi ya mwongo inazidi dhambi ya mlevi

Amesema al-Imam Muhammad al-Baqir a.s. katika *Usuli Kafi, Kitabul Iman wal-Kufr, mlango wa uwongo* : "*Bila shaka Allah swt ametengeneza kufuli kwa kila dhambi, na ufunguo wa kufuli hizo ni ulevi ambapo uwongo ni mbaya hata kuliko ulevi."*

Ulevi unaangamiza akili na fahamu lakini uwongo si kwamba unaangamiza akili na fahamu lakini unamfanya mtu akose adabu na heshima kiasi kwamba yeye huwa tayari kwa jambo lolote la kishetani. Mlevi atakapokuwa amelewa, huwa hana uwezo wa kuiharibu jamii kwani anakuwa hana fahamu wala habari zake mwenyewe lakini mwongo akiwa katika fahamu zake timamu huweza kuiharibu na kuiteketeza jamii nzima kwa hila na uwongo wake. Na hivyo kuleta hasara kubwa sana kwa jamii nzima.

Mdomo wa mwongo hunuka harufu mbaya

Zipo riwaya zisemazo kuwa Siku ya Qiyama midomo ya wasema uwongo itakuwa ikinuka harufu mbaya sana !.

Malaika pia wanachukizwa

Harufu mbaya iliyozungumzwa hapo juu, itakuwa mbaya kabisa kiasi kwamba hata Malaika Siku ya Qiyama watachukizwa kumkaribia huyo mwongo anayenuka harufu mbaya. Lakini si Siku ya Qiyama tu, bali hata humu duniani pia wanaisikia harufu mbaya ikitoka vinywani mwa wasema uwongo. Ipo Hadithi ya Mtume Muhammad s.a.w.w. isemayo : *"Wakati mja wa Allah swt anaposema uwongo, basi hutokwa na harufu mbaya kabisa kutoka mdomo wake kiasi kwamba hata Malaika pia wanajiweka mbali. nae" (Mustadrak al-Wasail.)*

Uwongo ni sababu za kufr:

Allah swt humlaani msema uwongo:*kama vile Aya ya Mubahila inavyoelezea* ***Sura An-Nuur, 24, Ayah ya 7*** *kama ilivyokwisha elezwa kuwa*

inadhihirisha waziwazi. '... Laana ya Allah iwe juu yake iwapo ni miongoni mwa waongo.'

Mwongo hunuka vibaya

Imepokelewa riwaya isemayo kwamba harufu mbaya inayotoka mdomoni mwa waongo hufika mpaka mbingu.

Malaika humlaani mwongo

Imepokelewa riwaya kuwa Malaika walio karibu ya Allah swt pia humlaani msema uwongo.

Uwongo huangamiza imani.

Amesema al-Imam Muhammad al-Baqir a.s. katika *Al-Kafi* : "*Uwongo ni kiangamizacho Imani.*"

Uwongo unamkosesha mtu asiweze kuionja imani.

Al-Imam 'Ali ibn Abi Talib a.s. amesema katika *Al-Kafi* : "*Mtu yeyote hataweza kuionja imani hadi hapo atakapoacha uwongo, ama uwongo huo uwe wa kikweli au kimzaha.*"

Uwongo unaleta chuki na uadui

moyoni mwa mtu ndivyo inavyopatikana kwa mujibu wa riwaya,.

Uwongo humwangusha mtu katika macho ya heshima na staha.

Ipo katika Hadithi moja ya Mtume Muhammad s.a.w.w. isemayo : "*Kwa mtazamo wa heshima na kiadabu, mtu aliye chini kabisa ni yule msema uwongo."*

Uwongo ni ufunguo wa mabaya

Imeripotiwa kuwa uwongo ni ufunguo wa kufuli ambayo imepigwa katika nyumba iliyofungwiwa maovu yote.

Uwongo ni ufasiki.

Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema katika *Mustadrak al-Wasail* kuwa : "*Jiepusheni na uwongo kwani hiyo ni mojawapo ya aina za ufiski, na vyote hivi viwili ni vitu vya Jahannam."*

Malaika elfu sabini wanamlaani mwongo

Ndivyo inavyo elezwa .

Uwongo ni alama ya unafiki.

Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema katika *Al-Mustadrak al-Wasail* kuwa : "*Zipo alama tatu za mnafiki : kusema uwongo, kufanya hiana na kugeuka ahadi alizozitoa."*

Ushauri wa mwongo kisheria haupendekezwi.

Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema katika *Al-Mustadrak al-Wasail* : *"Ushauri wa mwongo hauna umuhimu wowote."*

Uwongo ni ugonjwa mbaya kabisa wa kiroho.

Al-Imam 'Ali ibn Abi Talib a.s. amesema katika *Al-Mustadrak al-Wasail*: *"Na ugonjwa wa uwongo, ni ugonjwa mbaya kabisa wa kiroho."*

Uwongo ni urembo wa mkono wa Shetani.

Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema : *"Bila shaka Ibilisi hujipaka wanja, huvaa uchawi vidoleni na hutumia vyombo vya kuvutia hewa puani. Ama wanja wake kufanya ni visingizio na uvivu, ama uchawi*

wake vidoleni ni uwongo na chombo cha kuvutia puani ni takabari na ghururi !"

Katika anachojichumia mwanadamu uwongo ndio kitu kiovu kabisa..

Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema katika *Al-Mustadrak al-Wasail* : *"Mapato maovu kabisa ya mwanadamu, ni uwongo."*

Uwongo unawaingiza Motoni

Imeelezwa katika *Al-Mustadrak al-Wasail kuwa* Mtume Muhammad s.a.w.w. alijiwa na mtu mmoja aliyeuliza :*"Ewe Mtume Muhammad s.a.w.w. Je ni matendo yapi hasa yanawafanya watu waingie mtoni (Jahannam) ?"*
Mtume Muhammad s.a.w.w. alimjibu :*"Uwongo ! Iwapo mtu atasema uwongo, basi atakuwa amejiingiza katika dhambi ya uasherati, na hivyo amekufuru, na anayekufuru ataingia Motoni (Jahannam)."*

Mwongo huzalisha usahaulivu na upotofu.

Mwongo huugusa ugonjwa wa kusahau.

Amesema al-Imam Ja'afar as- Sadique a.s. katika *Wasa'il al-Shiah* : *"Kwa hakika mtu ambaye anapindukia kusema uwongo huadhibiwa adhabu ya kumuasi Allah swt ambavyo mojawapo ni ugonjwa wa usahaulivu !" Na hivyo ndivyo ilivyo kuwa mtu husema uwongo na mara husahau kama yeye alikuwa amesema uwongo na hatimaye uwongo wake hukamatwa na hivyo kudhalilika, na katika kujaribu kujitetea na kujihifadhi inambidi azungumze uwongo mmoja baada ya mwingine na hivyo huingia katika machachari ya kutaka kuulinda uwongo wa kwanza.*

Lakini hatambui kuwa kila asemavyo uwongo mmoja baada ya mwingine, anaendelea kujidhalilisha tu." Yaani mara nyingi tunajaribu kuunusuru uwongo hata wa kufika mia, bila hata ya kuona aibu, na hii

ndiyo laana ya Allah swt kwa msema uwongo. Hapa roho na akili yake vinamkataza, lakini wasiwasi wa Shetani unamburuza tu katika kusema uwongo baada ya uwongo kwani yeye anakuwa ni mfungwa wa Shetani.

Uwongo ni mlango mojawapo ya milango ya ufisadi na unafiki.

Msema uwongo huadhibiwa vikali

Msema uwongo huadhibiwa kwa adhabu mahususi. Mheshimiwa Rawandi katika kitabu chake *Da'awat* anaandika Hadith moja ndefu ya Mtume Muhammad s.a.w.w. katika maudhui haya ambayo inazungumzia vile alivyokuwa akisimulia Mtume Muhammad s.a.w.w. kile alichokiona katika Me'raj, kwamba :

"*Nilimkuta mtu mmoja amelazwa juu ya tumbo lake na yupo mtu mwingine ambaye amesimama juu ya kichwa chake na ambaye anayo nyundo ya misumari ambayo anampiga nayo yule mtu aliyelazwa na kumjeruhi. Uso wake unajeruhiwa kiasi cha kubomoka bomoka kabisa katika vipande vipande ! Nyundo inapoinuliwa juu mtu huyo huwa salama na punde inapoteremka chini hujeruhiwa na na hivyo ndivyo ilivyo kwa adhabu yake."*

Kwa hiyo Mtume Muhammad s.a.w.w. anasema kuwa : "*Mimi niliuliza ni sababu gani ya kuadhibiwa hivi ?"*

Alijibiwa : "*Huyu ni yule mtu ambaye alipokuwa akitoka nyumbani kwake, alikuwa akisema uwongo kiasi kwamba watu wa duniani walikuwa wakipata hasara kubwa kutoka na uwongo wake. Basi adhabu hii atabakia nayo hadi Qiyama."*

Mwongo hukosa sala za usiku wa manane (salatul Layl)

Na baraka zote zipatikanazo kwa sala hii huzikosa na baraka mojawapo ya sala hii ni kupatikana na kuongezeka kwa riziki. Bwana Sharif, anamnakili Al-Imam Ja'afar as- Sadique a.s. akiwa amesema, katika *Bihar al- Anwar* : "*Mtu anaposema uwongo hukosa baraka ya kusali*

sala za usiku wa manane na kama atakosa baraka za sala hiyo basi na baraka za riziki pia hukosekana !"

Uwongo ndiyo sababu ya kukosa hidaya na kujipatia upotofu

Allah swt anatuambia katika Qur'an Tukufu ***Sura Az-Zumr, 39, Ayah ya 3*** *: ' '..Bila shaka Allah hamwongozi aliye mwongo, aliye kafiri."*

Uwongo huondoa ubinadamu:

Mtume 'Isa ibn Maryam a.s. amesema , katika *Al-Kafi* : *"Mtu ambaye anakithiri kwa uwongo basi ubanadamu wake humwondokea." Na kwa hiyo huwa ana uhusiano na watu kwani na watu wenyewe huwa hawana moyo nae."*

Uwongo ni uovui na uchafu mkubwa.

Uwongo ni mojawapo ya dhambi kubwa (Dhunub Kabirah) kama ilivyokwisha thibitishwa hapo awali.

Uwongo upo mbali na imani bali tuseme kuwa ni kinyume cha imani.

Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema, katika *Al-Mustadrak al-Wasail* : "*Kila atakavyozidi kusema mtu kwa uwongo, basi ndivyo vivyo hivyo imani ya mtu itavyozidi kupungua !"*

Mwongo ndiye mwenye madhambi mengi kuliko wote.

Katika *Al-Mustadrak al-Wasail* ipo hadith ya Mtume Muhammad s.a.w.w. inayosema : *"Mojawapo ya dhambi kuu niya mtu mwenye mazungumzo na uwongo wa mtu kupindukia kiasi."*

Mwongo hujiteketeza kwa uwongo wake

Al-Imam ‘Ali ibn Abi Talib a.s. amesema katika *Al-Mustadrak al-Wasail* *“Jiepusheni na uwongo hata kama mtaona ufanisi ndani yake, lakini kwa hakika huo si ufanisi bali ni maangamizo ndani yake.”*

Mwongo hastahiki kuwa ndugu na rafiki wa watu

.Al-Imam ‘Ali ibn Abi Talib a.s. amesema katika *Wasa’il al-Shiah* : *“Inambidi kila Mwislamu asiufanye uhusiano na kiudugu na urafiki pamoja na msema uwongo aliyekithiri !”*
Akaendelea Al-Imam ‘Ali ibn Abi Talib a.s. kusema : *“Kwani rafiki wake mwongo pia huchukuliwa kuwa ni mwongo ! Kiasi kwamba hata kama atasema ukweli wowote, ukweli huo hautasadikiwa kuwa ni ukweli.”*

Allah swt hawaongozi wafujaji na waongo

Allah swt anatuambia katika Qur’an Tukufu ***Sura Al-Mumin, 40, Ayah ya 28*** kuwa *‘Kwa hakika Allah hamuongozi yule ambaye amepindukia mipaka na mwongo.’* Hivyo inamaanisha kuwa msema uwongo na mfujaji huwa wako mbali na haki na uhakika.

Mwongo huonekana kuwa ni binadamu, lakini sivyo

Ipo riwaya katika kitabu kiitwacho *‘Uyunil Akhbar ar-Ridhaa a.s.:* Kwa hakika mwongo huonekana kuwa ni binadamu lakini katika hali ya *Barzakh* hana uso wa kibinadamu. Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema akiwa anamwelezea Bi.Fatimah az-Zahra a.s. tukio la *Mi’raj*,: *“Usiku wa Mi’raj mimi nilimwona mwanamke mmoja ambaye kichwa chake kilikuwa kikifanana na kichwa cha nguruwe na mwili mzima uliobakia ulikuwa kama wa punda. Sababu ya hayo ni kuwa yeye alikuwa na tabia ya fitina na alikuwa akisema uwongo.”*

Daraja mbalimbali za uwongo

Kundi moja la Mujtahid kama alivyokuwa Shahidi Thani, wanasema kuwa dhambi hata ikiwa ya kiasi gani, lakini ni *dhambi kubwa*. Lakini kwa mujibu wa riwaya tunapata kujua kuwa uwongo unamadaraja mbalimbali na baadhi ya hizo kwa hakika ni *kubwa* na baadhi ya uwongo ni dhambi kubwa kabisa na baadhi ya uwongo unatilia shaka kuwepo kwake kuwa dhambi kubwa. Hivyo tunajaribu kuwachambulia daraja zake moja baada ya nyingine.

Kuwazulia uwongo Allah swt, Mtume s.a.w.w. na Maimamu a.s.

Uwongo muovu kabisa ni ule wa kuwazulia uwongo hao watajwa watatu hapo juu.
Allah swt anatuambia katika ***Sura An-Nahl,16, Ayah ya 116 na 117 :***
‘ Na msiseme kwa sababu ya uwongo usemao midomo yenu, hili ni halali na hili ni haramu ili msije mkamzulia uwongo Allah. Hakika wale wanaomzulia uwongo Allah , hawatafanikiwa.’

‘(Duniani) Kuna faida kidogo tu lakini (Aakhera) watapata adhabu kali zinazo umiza.’

Amesema al-Imam Ja’afar as- Sadique a.s. katika *Al-Kafi* :
“*Kuwazulia uwongo Allah swt na Mtume Muhammad s.a.w.w. ni dhambi Kubwa (dhamb kabirah).”*

Amesema al-Imam Ja’afar as- Sadique a.s. katika *Al-Kafi*:
“Msituzulie hata uwongo mmoja kwanikufanya hivyo kutakutoeni nje ya Dini hii bora ya Uislamu.” Yaani kwa kuwazulia Maimamu a.s. uwongo hata mmoja kunatokomeza nuru ya Imani kutoka moyoni mwa waongo. Iwapo uwongo kama huu utazuliwa kwa Maimamu a.s. katika hali ya saumu, basi saumu inabatilika papo hapo.

Uwongo hata ukiwaje

Uwongo hata ukiwaje na kwa hali yeyote ile, ni haramu kabisa. Kama ilivyoharamishwa kusema uwongo, basi na kuandikwa uwongo pia kumeharamishwa. Hata kiasi cha kuonyesha kwa kidole au kutikisa kichwa katika kufanya ishara ya kuelezea uwongo pia kumeharamishwa. Mfano, iwapo mtu hakusali na kama akiulizwa, je umesali ? naye kwa kutikisa kichwa akajibu kuwa '*naam nimesali*', basi hivyo pia ni haramu. Vile vile iwapo kuna mtu anasema uwongo na wewe unatambua hivyo lakini unamuunga mkono katika uwongo wake, hivyo pia ni uwongo na ni haraamu. Au kumlinda mtu katika uwongo pia ni haramu.

Vile vile ni dhambi kubwa kwa kuwazulia na kuwanasibisha Allah swt , Mtume Muhammad s.a.w.w. na Maimamu a.s. uwongo wa aina yoyote ile, na Kutafsiri aya za Qur'an Tukufu na ahadith kwa kuzua Mfano:

- Kwa kujua kuwa jambo fulani halikusemwa na Mtume Muhammad s.a.w.w. lakini wewe ukamzulia yeye hilo jambo kuwa '…. Hivi ndivyo alivyosema Mtume Muhammad s.a.w.w..'
- Vile vile kunaweza kuwepo kifungu cha maneno ya Kiarabu, wewe ukaisema kuwa hiyo ndiyo Ayah ya Qur'an Tukufu
- Vile vile kutafsiri Ayah ya Qur'an Tukufu au hadithi kwa mujibu wa maslahi ya mtu mwenyewe au tuseme kujitolea maana kwa faida yake mtu mwenyewe.

Kazi maalumu kwa watu maalumu

Kukaa juu ya *Mimbar* au kutafsiri na kutarjumu Ayah za Qur'an Tukufu ni shughuli moja nyeti mno na hivyo si kazi ya kila mtu na inahitaji uangalifu mkubwa sana na tahadhari za kila aina. Iwapo mtarjumi au mfasiri wa Ayah za Qur'an Tukufu na hadithi hakusomea elimu ya Kiarabu kwa nahau na sarufi, basi lazima atatoa maana isivyo na hivyo ni hatari sana kwani hataweza kuepukana na makosa hayo. Hivyo

makhatibu na waandishi wanatahadharishwa sana kuwa wasitoe maana vile watakavyo isipokuwa watoe maana iliyo dhahiri na wazi kabisa. Hususan wajiepushe na kutafsiri na kutarjumu Ayah za Qur'an Tukufu zilizo *mutashabih* .

Mfano wa kumzulia uwongo Allah swt

Ni jambo la kawaida kwetu sisi kusema : "*Allah swt yupo shahidi kuwa kile nikisemacho ni sahihi au Allah swt anajua kuwa kile nikisemacho ni kweli Utupu."*

Amesema al-Imam Ja'afar as- Sadique a.s. katika *Al-Kafi* :

> *" 'Mtu yeyote atakayesema kuwa Allah swt anajua' wakati Allah swt anajua asili (yaani kinyume na anachodai huyo mtu kwa kutenda kinyume) basi 'arsh-i-Ilahi inatetemeka kwa kuona Ukuu wa Allah swt unasingiziwa."*

Vile vile Amesema al-Imam Ja'afar as- Sadique a.s. katika *Wasa'il al-Shiah ,Kitabul Iman, mlango na.5* :

> *"Iwapo mtu atasema kuwa 'Allah swt anajua wakati yeye ni mwongo' basi Allah swt anamwambia 'je ewe hukumpata mwengine wa kumdanganya isipokuwa Mimi tu? Ambaye unamzulia uwongo ?"*

Kwa mujibu wa riwaya nyingine, inasema kwamba wakati mtu anapomfanya shahidi Allah swt katika uwongo anaouzua, basi Allah swt humwambia : *"Je hujampata mdhaifu mwengine yeyote kuwa shahidi wako katika uwongo na uzushi wako huo isipokuwa umenipata Mimi tu ?"*

Kuzua uwongo dhidi ya Mtume Muhammad s.a.w.w. na Maimamu a.s.

Kuwazulia Mtume Muhammad s.a.w.w. na maimamu a.s. kunamaanisha kuwa mtu anajitungia hadithi yake mwenyewe kuwanasabisha hao watukufu na vile vile kwa kujua waziwazi kuwa hadith aijuayo ni ile ambayo imezuliwa (siyo sahihi) lakini kwa

makusudi anaileta kwao. Lakini iwapo hadithi aliyonayo ni sahihi na kweli, basi anaweza kuwanasabisha nayo Mtume Muhammad s.a.w.w. na Maimamu a.s.

Riwaya zitolewe pamoja na nyororo za mapokezi

Katika vitabu vingi tunaona na kusoma hadithi na riwaya nyingi ambazo zimeandikwa bila ya kuonyesha nyororo za mapokezi, hivyo inatutia wasiwasi kuhusu usahihi wa hadithi. hizo au ni zile ambazo zimezuliwa na kutengenezwa. [2] Iwapo kutakuwapo na dharura ya kuziandika hadithi kama hizo, basi kunaweza kuandikwa jina la kitabu au na jina la aliyeipokea na kuinakili. Kabla ya kuandika Hadith inabidi kuangalia kwa makini kuwa Hadith hizo haziendi kinyume na maamrisho ya Dini ya Uislamu na iwapo itaonekana kuwa Hadith hiyo ni kinyume na kanuni za Dini ya Uislamu basi lazima Hadith hizo ni za kuzuliwa na kuundwa. Jambo la kuzingatia ni kwamba katika Hadith zote hizo kamwe kusiwepo na uwazi wala ishara ya kuwakashifu Mtume Muhammad s.a.w.w. na Maimamu a.s. vile vile kusiwepo na mambo yoyote yale yanayopingana na akili zetu au akili zetu zikatae kuzikubali. Na ni ushauri kuwa mtu inambidi atoe hadithi kutoka vitabu ambavyo vinaaminiwa na kutegemewa vyema.

Amesema al-Imam Muhammad al-Baqir a.s. katika *Kashaful Hujjat* :

> *"Kamwe musinakili hadithi kutoka mtu ambaye hategemewi ama sivyo wewe utakuwa umesema uwongo mkubwa kabisa,,.na mwongo ni mtu aliyedhalilika mbele ya Allah swt na viumbe vyake."*

Al-Imam 'Ali ibn Abi Talib a.s. alimpa nasaha Harith Hamdani kwa barua aliyokuwa amemwandikia: (rejea Nahjul-Balagha):
"Usiwe nimwenye kuwaambia watu yale yote uliyoyasikia, kwani kunatosheleza katika kusema uwongo."

Vile vile inatakiwa wakati wa kutoa hadithi, kunakiliwe vyema *min* (kutokea) na *'an* (kwa mamlaka ya) wala haistahiki kuongeza au kupunguza chochote wala haitakiwi kubadilisha herufi hata moja ama sivyo kuna hatari ya kuwasingizia Ma'asumiin a.s.

Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema, katika *Wasa'il al-Shiah* : *"Mtu yeyote atakacho ninasabia kile ambacho sijakisema, basi makao yake yatakuwa ni Jahannam (Motoni) tu."*

Bwana Nuuri katika kitabu chake *Darus-Salaam* anaandika kuwa Bwana mmoja aliye elimika na mwenye matendo, mema kwa ajili ya kukisanifu kitabu *maqame'* alimwendea Bwana Muhammad 'Ali huko Karmanshah na kusema : "*Mimi nimeota usingizini kuwa ninaiparua nyama ya al-Imam Husayn ibn 'Ali ibn Abi Talib a.s., sasa je nini utabiri wa ndoto hii ?"*

Bwana Muhammad 'Ali aliinamisha kichwa chake na kufikiria, baada ya punde akasema : *"Bila shaka wewe ni khatibu wa kusoma Majlis na kusoma masaibu."* Huyo Bwana akajibu *: "Naam* !" Akamwambia : *"Ama shughuli hii uiache au usome kwa kutoa maudhui yako kutoka vitabu vinavyo aminiwa na kutegemewa kwa usahihi."*

Imeandikwa katika kitabu *Shifaus-Suduur* kuwa siku moja Shekhe mmoja alikuwa akisoma waadhi mbele ya Ayatullah al-Haj Muhammad Ibrahim Kalbasi. Sheikh huyo alikuwa akionyesha kuwa al-Imam Husayn ibn 'Ali ibn Abi Talib a.s. alisema "*Ya Zainab! Ya Zainab !"* kwa kuyasikia hayo Ayatullah Kalbasi akasema kwa sauti kubwa : "*Allah swt auvunje uso wako ! Al-Imam Husayn ibn 'Ali ibn Abi Talib a.s. hakusema mara mbili, badala yake alisema mara moja tu !"*

Kuelezea madhumuni ya riwaya

Ingawaje kunaruhusiwa kuelezea mafuhumu na madhumuni ya Ayah ya Qur'an Tukufu au hadithi katika maneno ya mtu mwenyewe lakini kuna baadhi ya masharti kama vile msemaji huyo lazima awe anajua vyema lugha ya Kiarabu na vile vile awe stadi katika kujua na kuelewa. Kwa kifupi tunaweza kusema kuwa yeye anaruhusiwa kueleza mafuhumu katika maneno yake kwa ufasaha wa hadithi hizo.

Vile vile iwapo hakutakuwa na hatari ya kuwasema kiuwongo, Ma'asumiin a.s. basi anaweza hata kubadilisha katika kimashairi vile

vile matukio yaliyopita nyakati za nyuma yanaweza kusemwa katika wakati uliopo mfano unaweza kusema kuwa mtu mmoja alimjia Imam a.s. na Imam a.s. alimwambia. Hivyo katika kuzungumzia katika wakati tuliopo inawezekana kusema kuwa 'mtu mmoja anamjia Imam a.s. na Imam a.s. anamwambia'. Lakini wasikilizaji inawabidi waelewe kuwa hayo yanayozungumzwa ni katika wakati uliopo. Iwapo itakuwa 'Imam a.s. alikataza' kwa hiyo katika maneno yake anaweza kusema kuwa 'Imam a.s. amesema musifanye hivyo '.

Kujiepusha na viapo viongo na ushahidi wa kiwongo

Daraja moja lingine la uwongo ni kule kula kiapo cha uwongo, kutoa ushahidi wa uwongo au kuficha ushahidi katika Mahakama ya *Shariah*. Hakuna shaka kwamba huo ndio uwongo ambao umo katika Madhambi makubwa Insha Allah yote hayo yatazungumzwa kiundani ili kueleweka vyema.

Athari mbaya za uwongo

Kwa hakika uwongo unakuwa na athari mbaya na huleta hasara kwa mwongo na wengine pia, ndio maana umeharamishwa na ni *dhambi Kuu*. Vile vile ukubwa na wingi wa adhabu kwa kusema uwongo unategemea vile unavyoathiri mfano adhabu ya kusema uwongo ukampa hasara ya mali itakuwa kidogo ya kuuawa kwa mtu.

Uwongo kwa kusema katika kicheko na mzaha

Uwongo pia huwa na aina moja ambapo msema uwongo huzungumza katika hali ya mzaha; mfano, iwapo mtu mmoja mpole akiambiwa kuwa mwanamke fulani yupo tayari kuolewa nawe au mtu fulani amekualika chakula cha usiku nyumbani kwake ambavyo kwa hakika hakuna jambo kama hili.

Aina hii ya uwongo wa mzaha pia umeharamishwa kwa sababu ndivyo inavyopatikana kwa mujibu wa riwaya. Lakini Maulamaa wanasema

kuwa uwongo kwa kweli kama unadhihirisha maana yake kuwa ni mzaha basi inaruhusiwa, mfano iwapo mtu asiyeoa akiambia angalia mke wako anakwenda, basi hivyo si haraam. Yaani msikilizaji hahadaiwi kwa yale ayasikiayo. Lakini ikumbukwe waziwazi kuwa iwapo kutakuwapo na hatari ya kuhadaiwa, basi itakuwa ni haramu kufanya mzaha kama huo. Ingawaje baadhi ya Mujtahid wanaharamisha uwongo katika mzaha. Bila ya kujali iwapo udhahiri wake utaonekana au la hiyo ndivyo njia ya kujiepusha na kujitahadharisha na vivyo hivyo ndivyo inavyopatikana katika riwaya.

Kujiepusha na uwongo kwa kikamilifu

Amesema al-Imam Zayn-al-'Aabediin a.s. katika *Al-Kafi:*

> *"Jiepusheni na uwongo, ama iwe mdogo au mkubwa, au uwe katika hali ya masikitiko au huzuni au katika mzaha."*

Al-Imam 'Ali ibn Abi Talib a.s. amesema katika *Al-Kafi* :

> *"Mtu yeyote hawezi kamwe kuionja Imani yake hadi hapo atakapo jiepusha na uwongo, haidhuru kama utakuwa katika huzuni au mzaha."*

Imeelezwa kutoka Al-Imam 'Ali ibn Abi Talib a.s. amesema katika *Wasa'il al-Shiah* :

> *"Hakuna wema katika uwongo hata kama utakuwa katika hali ya huzuni au furaha. Wala hautakiwi kutoa ahadi za uwongo kwa watoto wako, ahadi ambazo huna nia ya kuzitimiza. Kwa hakika uwongo unampotosha mtu kutenda madhambi makubwa makubwa ambayo hatima yake humtumbukiza mtu katika Moto wa Jahannam."*

Mtume Muhammad s.a.w.w. alipokuwa akimusia Abu Dhar al-Ghaffari,alimwambia :

> *"Ewe Abu Dhar ! Mtu yeyote atakaye jihifadhi dhidi ya uharamisho sehemu zake za siri na ulimi wake, basi ataingia Peponi. Mtu yeyote atakayetamka uwongo katika mzaha basi uwongo huo katika mzaha utampeleka hadi Jahannam !"*

"Ewe Aba Dhar ! Ole wake yule mtu ambaye anapozungumza huzungumza uwongo ili aweze kuwachekesha watu. Ewe Abu Dhar ! Yule ambaye atakayekaa kimya ataongoka. Hivyo kukaa kimya kwako ni faradhi kuliko kunasibisha uwongo na kusitoke kamwe uwongo hata kiasi kidogo kutoka kinywani mwako."

Bwana Abu Dhar anasema:

"Je tawba ya mwenye kusema uwongo kwa kujua hivyo, itakuwaje ?"

Mtume Muhammad s.a.w.w. alisema katika *Wasa'il al-Shiah*

"Kufanya Isteghfar na kusali sala tano kwa kutimiza masharti yake ndiyo yanayoweza kuyaosha madhambi hayo."

Vile vile Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema katika *Jihad* :

"Laana ya Allah swt inamwia msema uwongo hata kama atasema katika mzaha"

Vile vile Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema, katika *Al-Khisal* :

"Mimi ninachukua dhamana ya kumpatia nyumba katika daraja iliyo ya juu kabisa katika Jannat kwa ajili ya mtu yeyote ambaye anajiepusha na ugomvi na vita halafu hata kama yeye atakuwa katika haki. Na nitampatia nyumba mtu yeyote yule katika daraja iliyo ya kati ambaye anajiepusha kusema uwongo hata kama atakuwa katika mzaha. Na vile vile nitampatia nyumba katika bustani za Jannat kwa mtu yeyote yule mwenye tabia njema."

Uwongo usemwao katika hali ya mzaha ni dhambi lakini si *dhambi kubwa* Lakini iwapo kusema uwongo katika hali ya mzaha itaweza kumdhuru mtu kwa kumkashifu au kumdhalilisha au kumpatia hasara ya hali na mali au hadhi yake au kumdhuru kimwili au kidhahiri au kichini chini basi katika sura hizi, uwongo huu katika mzaha utakuwa ni *dhambi kubwa* .

Kurejea si uwongo

Katika mazungumzo ya kawaida, kuongezea si uwongo. Mfano utamsikia mtu baada ya kuelezea jambo fulani mara chache, utamsikia akisema kuwa ameshasema jambo hilo mara mia moja, lakini kwa hakika hakusema mara mia moja. Na huu si uwongo bali yeye anajaribu kuelezea kuwa amekwishalieleza mara nyingi sana kupita kiasi na ni jambo la kutilia mkazo tu.

Tusidhanie kila uwongo kuwa ni 'mdogo tu'

Mara nyingi tunaona kuwa mtu anapokuwa akiulizwa na mwenyeji wake kuwa ale chakula, lakini mgeni pamoja na kuwa na njaa hujibu *hapana mimi sina njaa* ambapo kwa hakika anakuwa na njaa, basi huu ni uwongo ! Kwa hakika watu wanaona jibu hilo kuwa ni jambo la kawaida tu na hawalijali wakati Shariah inasema kwa mujibu wa *riwaya* kuwa huo ni uwongo na ni haramu.

Imepokelewa riwaya kutoka *Safinatul Bihar, j.2, uk. 473* kuwa Asma' binti 'Umays anasema, :

> *"Usiku wa kwanza wa 'Aisha, Mtume Muhammad s.a.w.w. alinipa chombo kimoja cha mazima akisema 'wape wanawake wanywe'*
>
> Wanawake wakasema *: 'Sisi hatuna njaa' Mtume Muhammad s.a.w.w. kwa kuyasikia hayo alisema :'Njaa pamoja na Uwongo musivichanganye pamoja !"*

Asma' akauliza :

> *"Iwapo sisi tutakuwa tukitamani au tukitaka kitu na tukasema kuwa hatukitaki au hatukitamani, basi jee huo ni uwongo ?"*

Basi Mtume Muhammad s.a.w.w. alimjibu :

"Naam ! Bila shaka kila aina ya uwongo unaandikwa kiasi kwamba hata uwongo mdogo mdogo pia huitwa uwongo."

Iwapo mtu kwa heshima kamkaribisha mtu nyumbani kwake kwa kusema "Karibu bwana nyumbani kwangu", lakini moyoni mwake hataki huyo mtu aje nyumbani mwake., huu sio uwongo. Kwa sababu neno *karibu* haliwezi kusemwa kuwa ni neno la *ukweli au uwongo*. Hata hivyo kunashauriwa kuepukana na kujionyesha hivi. Kwa hakika hali hii yaonyesha jambo lililo mdomoni ni tofauti na lile lililo moyoni, na huo ndio unaoitwa *unafiki*.

Ipo riwaya moja kutoka kitabu *Bihar al- Anwar , j. 16, mlango wa hishima ya ndugu mu'miin ..., uk. 241* ipo riwaya ifuatayo :

Siku moja al-Imam Ja'afar as- Sadiq a.s. alikuwa ameketi pamoja na mwanae Isma'il, na akaja mfuasi wake mmoja akatoa salaam na akaketi pamoja nao. Wakati Imam a.s. alipoondoka kuelekea nyumbani mwake, basi na yule mtu pia akaondoka kumfuata Imam a.s. hadi kizingitini mwa nyumba ya Imam a.s. Imam a.s. hapo hapo aliagana nae na kuingia nyumbani mwake, mwana wa Imam a.s., Isma'il alimwuliza babake ni kwa nini hakumkaribisha mtu huyo kuingia nyumbani mwao kama desturi njema ? Imam Ja'afar as- Sadiq a.s. alimwambia kuwa haikuwa munasibu kwa mtu yule kuingia ndani, kwani mimi binafsi sikuwa nataka huyo mtu aje ndani na wala sikutaka Allah swt anihesabu miongoni mwa watu ambao wanasema nini mdomoni mwao na wanavyo nini mioyoni mwao !"

Uwongo wa ndoto

Kuna aina moja nyingine ya uwongo kuwa *"Mimi nimeota hivi na hivi ..?" au kumsingizia ndoto mtu mwingine kuwa fulani bin fulani ameota hivi na hivi."* Kwa hakika hii nao ni uwongo.

Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema kuwa **uwongo Mkuu** upo katika makundi matatu **:**

·*Kumwita mtu kwa jina mbali na jina la mzazi wa kweli.*
·*Kusema ndoto za uwongo ambazo hakuziota,*

·Au aseme kile ambacho mimi (Mtume Muhammad s.a.w.w.) sikusema..

Kuna aina nyingine ya uwongo ni kule kuzua visa. Visa ambavyo havina misingi lakini vinasadikiwa. Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema katika *Bihar al- Anwar, j.15, uk. 42* kuwa : *"Uwongo ulio muovu kabisa ni kunakili kwa riwaya zilizo za uwongo."*

Uwongo katika kutoa mifano

Mara nyingi hutolewa mifano katika kuelewesha jambo fulani. Na mojawapo ya mifano inayozungumziwa ni kule wanayama wakizungumza miongoni mwao (kuwa wanyama wanazungumza) lakini kwa hakika sote tunajua kuwa wanyama hawazungumzi, na hivyo ni wazi kuwa hakuna mtu anayedanganyika kwa mfano huo bali anafaidika tu, hivyo mazungumzo kama haya yanaruhusiwa. Vile vile sisi tunapata riwaya kama hizi katika maisha na mazungumzo ya Ahlul Bayti a.s. ya Watoto wa Mtume Muhammad s.a.w.w. ambapo kwa kutolewa mifano kama hiyo kunabadilisha mazungumzo na kutoa nasiha na kuelezea uhakika, na ndiyo maana vimeruhusiwa.

Al-Imam Husayn ibn 'Ali ibn Abi Talib a.s. atoa mfano

Siku moja al-Imam Husayn ibn 'Ali ibn Abi Talib a.s. alikuwapo katika baraza la Mua'wiyah na hapo mtu mmoja akaanza kutamka maneno yenye kashfa dhidi ya al-Imam Husayn ibn 'Ali ibn Abi Talib a.s..

Al-Imam Husayn ibn 'Ali ibn Abi Talib a.s. alimjibu :

"Ewe 'Umar ibn 'Uthman ! Tabia yako ina upumbavu ambao wewe hauwezi kuuelewa. Mfano wako ni kama ule wa mbu ambaye akijiona mkubwa aliukalia mtende na wakati wa kutaka kuruka, aliuambia mtende : 'jizatiti kwa umadhubuti, kwani sasa ninaruka kwa ajili ya kuteremka !' Kwa hiyo mti ukamjibu : 'Mimi wala sijui ni kutoka wakati gani umenikalia juu, sasa hebu niambie kuondoka kwako kutaniangusha ?!"

Kusikiliza uwongo pia ni haramu

Tuelewapo kuwa jambo lililopo ni uwongo basi na kulisikiliza pia ni haram. **Kama vile kuandika na kusomwa maandishi ya uwongo umeharamishwa basi na kunakili uwongo pia umeharamishwa.** Kwa hakika Qur'an Tukufu imekuwa ikiwalaumu Mayahudi na Makafiri kwa kupeleka habari za uwongo, za huku kupeleka huko na za huko kuleta huku.

As-Shayk Sadduq (a.r.) ameinakili riwaya ifuatayo kutoka kwa al-Imam Ja'afar as- Sadiq a.s. kuwa al-Imam a.s. aliulizwa :

"Je inaruhusiwa kusikiliza uwongo wa waongo kwa makini ?"

Amesema al-Imam Ja'afar as- Sadiq a.s. katika kumjibu (*Kitab-i-'itiqadat)* :

"Hapana ! Iwapo mtu anamsikiliza kwa hamu na basi huwa anafanya ibada kwa mujibu wake. Iwapo msemaji anamwamini Allah swt basi msikilizaji atafanya ibada ya Allah swt . Na iwapo msemaji anafuata maneno ya Shetani basi msikilizaji atafanya ibada ya Shetani."

Ipo riwaya kama hii ambayo inapatikana katika *Kitab Al-Kafii* kutoka al-Imam Muhammad al-Baqir a.s..

Allah swt anatuambia katika Qur'an Tukufu ***Surah Haj, 22, Ayah ya 30*** : *"Mjiepushe na maneno ya upuuzi"*

Allah swt anatuambia katika Qur'an Tukufu ***Surah Furqan, 25, Ayah ya 72****: 'Na wale ambao hawashuhudii shahada za uwongo…'*
Kwa mujibu wa Ayah kama hizi inadhihirisha kwambakusikiliza uwongo ni haramu. Bila shaka kuwa mahali panaposemwa uwongo na kumuasi Allah swt ni mahali ambapo watu hufanya uwasi kwa Allah swt na msikilizaji iwapo yupo hapo ameshirikiana nao basi atashirikiana nao katika madhambi hayo. Na kwa mujibu wa sheria vile vile ni faradhi kwa msikilizaji kutekeleza amri ya *Nahyi 'anil munkar* yaani kuzuia maovu ili muongo asiendelee kusema uwongo.

Je 'Tawriyyah' ni nini ?

Tawriyyah inamaanisha kusema jambo moja likawa na maana mbili. Yaani maana moja ikawa sahihi na ile ya pili ikawa inapingana na ukweli. Yaani inasemekana kuwa msema *tawriyyah* husema kwa nia ya kusema jambo sahihi lakini ni msikilizaji ndiye anayetoa maana iliyo kinyume na uhakika.

Mfano, iwapo atakuja mdhalimu mmoja nyumbani kwako na akakuita utoke nje, nawe hutaki, hivyo unajaribu kujihifadhi basi unabakia umejificha na mmoja wa watu wako akaenda mlangoni na kumwambia : "*Yeye hayupo hapa"* yaani unakuwa umemaanisha kuwa wewe hupo karibu na mlango ule. Na hivi huruhusiwa iwapo dhalimu ataelewa kuwa wewe hupo nyumbani humo.

Iwapo dhalimu atakuuliza mahali alipo mtu fulani ili akimwendea atamfanyia dhuluma, basi wewe unaweza kumjibu yeye : *"Mimi sijui anwani yake"* hapa neno *anwani yake* wewe unatambua wazi kuwa hujui kwa kweli anwani ya mtu anayeulizwa.

Iwapo wewe umetenda dhambi, (hatumuombi Allah swt hivyo), yoyote na mtu akakuuliza *"Je wewe umewahi kutenda dhambi kama hii?"* Basi wewe utasema hivi kwa kulinda heshima yako : *"Astaghfirullah ! Mimi nitamuomba Allah swt aniokoe iwapo nitatenda dhambi kama hiyo.",* Wewe unaweza kutumia maneno au maswali katika kumjibu, mfano unaweza kumjibu katika kumuliza *"Je unanitegemea mimi hivyo?"* Au unaweza kuomba dua *"Namuomba Allah swt anihifadhi na madhambi kama hayo."*

Iwapo wewe ulimwambia mtu siri ya aibu yako, naye akaona vibaya na kukununia, basi wewe hautakiwi kumwambia kuwa wewe haukufanya hivyo yaani wewe hauna aibu hiyo. Isipokuwa kwa ajili ya kumbembeleza, unaweza kusema : *"Wewe ni shakhsiyyah ambaye hautakiwi kuambiwa maneno kama haya."*

Hukumu za ‘tawriyyah’

Zipo aina tatu za *Tawriyyah* :

1. Aina ya kwanza :

Aina ya kwanza ni kwamba kuwepo na swala lililojotokeza au kujiepusha na hasara fulani. Mifano yake tumezungumzia hapo juu. Hapa hapana shaka ya aina yoyote kuwa aina hii ya *tawriyyah* imeruhusiwa.

2. Aina ya pili :

Aina ya pili ni kule kwa mtu kufanywa *tawriyyah* kwa ajili ya kutaka kumfikishia mtu mwingine hasara au kumfikishia shida au kumkashifu. Kwa hakika aina hii ni haramu.

3.Aina ya tatu :

Aina hii ya *tawriyyah* ni kwamba humo hakuna suala lililojitokeza wala hakuna kusudi la kumdhuru mtu yeyote. Baadhi ya *Mujtahid* wanasema kuwa aina hii ya tawriyya ni haraam. Kwa sababu *tawriyyah* ni aina mojawapo ya uwongo na hivyo kwa sababu zilizofanya uwongo kuwa haram ndivyo vivyo hivyo hivyo kunathibitishwa kwa *tawriyyah* kuwa haraamu. Na ieleweke kuwa hakuna mifano ya kuihalalisha aina hii ya *tawriyyah*. Vile vile wapo baadhi ya *Mujtahid* ambao wanasema kuwa aina hii ya *tawriyyah* si haramu. Kwa kupitia dalili zote zilizohalalisha tarwiyyah, ndizo hizo hizo zinazotumika kuihalalisha. Na hivyo ni dhahir kuwa *tawriyyah* si uwongo.

Hivyo inambidi mtu kufanya *tawriyyah* pale ambapo anaona kumeruhusiwa kwa yakini.

Mahali ambapo kusema uwongo umeruhusiwa

Popote pale ambapo kutakuwa na hatari ya maisha, mali au heshima ya mtu na kama kwa kusema uwongo kutamwondolea hatari hizo basi kunaruhusiwa kusema uwongo katika sura hizo. Hatari hizo ama ziwe kwa ajili yake mwenyewe au kwa ajili ya mtu mwingine. Hata hivyo imeruhusiwa kula kiapo cha uwongo kwa ajili ya kunusuru hayo. Katika baadhi ya nyakati, ni faradhi kusema na kula kiapo cha uwongo katika kuyanusuru maisha ya mtu, mfano, iwapo dhalimu atataka kumuua Mwislamu, anataka kumpiga na kumdhuru Mwislamu, au anataka kumdhalilisha na kumkashifu, anataka kumdhulumu na kumnyang'anya mali yake au anataka kumfunga mahabusu. Sasa iwapo huyo mdhalimu akikuomba anuwani ya Mwislamu huyo, basi ni faradhi kwako kutompatia anuwani yake, halafu hata kama itakubidi useme uwongo na ule kiapo cha uwongo kuwa wewe hujui chochote.

Iwapo wewe utakuwa na amana ya mtu na mdhalimu atakutaka umpatie hiyo amana ili umdhulumu huyo mtu, basi wewe unatakiwa katika kila hali uinusuru hiyo amana hata kama itakubidi uchukue msaada wa kusema uwongo na kula kiapo cha uwongo.

Kiapo cha uwongo kwa ajili ya kuwanusuru Waislamu

Kwa ajili ya kuwanusuru Waislamu kama itahitajika kula viapo vya uwongo, umeruhusiwa na zipo riwaya nyingi.
Sheikh Ansari anawanakili Al-Imam 'Ali ibn Abi Talib a.s. na al-Imam Ja'afar as- Sadiq a.s. katika *Makasib* kuwa Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema , *Wasa'il al-Shiah ,Kitab al-Iman, j. 3, mlango na. 12*:

> *"Mnaweza kula kiapo cha uwongo lakini mumnusuru ndugu yenu Mwislamu asiuawe bure !"*

Ismail Ibn Sa'ad ambaye Hadith yake ni sahihi anasema katika *Wasa'il al-Shiah , Kitabul Iman, j. 3, nambari 12* :

"*Mimi nilimwuliza Al-Imam 'Ali ar-Ridha a.s. kuhusu mtu ambaye amekula kiapo cha uwongo mbele ya mfalme kwa ajili ya kutaka kuinusuru mali yake."*

Al-Imam 'Ali ar-Ridha a.s. alimjibu :

"Hakuna shida yoyote."

Mwandishi anasema kuwa yeye alimwuliza tena Al-Imam 'Ali ar-Ridha a.s. :

"Je inaruhusiwa kwa mtu kula kiapo cha uwongo kwa ajili ya kunusuru mali ya Mwislamu mwenzake kama vile alivyokula kiapo cha uwongo kwa ajili ya mali yake mwenyewe?"

Al-Imam 'Ali ar-Ridha a.s. alimjibu:

"Naam ! Inaruhusiwa."

Al-Imam Ja'afar as- Sadiq a.s. anasema katika *Faqiyyah* :

"Iwapo itambidi Mwislamu kula kiapo cha uwongo kwa ajili ya kumnusuru Mwislamu mwenzake pamoja na mali yake isichukuliwe na mdhalimu au mwizi, basi hakuna shida ndani ya kula kiapo cha uwongo na si hayo tu, bali hatatakiwa kulipa kafara ya kula kiapo cha uwongo na badala yake atapewa malipo mema sana pamoja na thawabu nyingi mno kutoka kwa Allah swt."

Hasara ya mali na uwongo

Hapa itatubidi tuwe na mambo mawili akilini mwetu :

Kwanza : Kama tulivyokwisha ona kuwa kwa kila hasara ya mali, tunaweza kusema uwongo ili kuinusuru na hivyo imeruhusiwa

Vile vile iwapo ataweza kuvumilia hasara basi **ni Sunnah** kuvumilia na hivyo **asiseme uwongo.** Al-Imam 'Ali ibn Abi Talib a.s. amesema katika *Nahjul-Balagha,* kuwa :

"Ni alama ya Imani kuwa mtu aseme ukweli tu hata katika wakati wa kupatwa na hasara na asiseme uwongo kwa ajili ya kupata faida."

Afanye Tawriyyah kiasi awezacho

Pili : Vile vile lipo jambo lingine ambalo inatubidi kulitafakari vyema akilini mwetu, kuwa Mujtahid wanasema kuwa *tawriyyah* ni lazima na kwa kumalizia masuala yetu basi tuepukane na kusema uwongo badala yake inatubidi kufanya *tawriyyah*.

Kuwasuluhisha Mumini wawili kwa kutumia uwongo

Al-Imam Ja'afar as- Sadiq a.s. amesema katika *Wasa'il al-Shiah, Kitab Haj* :

"Mazungumzo yapo aina tatu :

- *Ukweli*
- *Uwongo*
- *·Kuwasuluhisha watu*

Kuna mtu aliuliza :"*Mimi niwe fidia kwako ! Je kuwasuluhisha watu ni kitu gani ?*

Al-Imam Ja'afar as- Sadique a.s. alimjibu :

"Wewe umsikie mtu mmoja akimzungumza na mtu mwingine na ukamwambia mtu mwingine kuwa fulani bin fulani alikuwa akikuzungumza vyema kabisa (ambapo kwa hakika ni kinyume chake kabisa) "

Ujumbe mkali

Kwa kifupi ni kwamba, iwapo itambidi mtu kuzungumza uwongo kwa ajili ya kutaka kuwasuluhisha au kuwapatanisha watu wawili na kupunguza makali baina yao, basi anaruhusiwa kutumia msaada wa uwongo na mtu kama huyu hataingia katika madhambi na aina hii inaitwa usuluhisho. Iwapo mtu ataufikisha ujumbe wenye maneno makali kwa mtu mwingine, basi kunaweza kutokea uhasama na uadui mkubwa zaidi.

Vile vile iwapo bibi na bwana wamekwisha tengana na umefika wakati wa *talaqa* basi inambidi mtu azungumze hata uwongo ilimradi aweze kuwasuluhisha, na kwa hakika hili ndilo litakuwa jambo jema kabisa.

Mtu anaweza kumwendea mume na kumwambia kuwa *"Loh ! Mke wako kwa kweli anasikitika mno kwa kuachana kwani anakupenda kupita kiasi na hivyo hataweza kuvumilia kuachana kwenu na anaweza kuugua."*

Na vivyo hivyo amwendee bibi na kumtengenezea mambo kama hayo ya uwongo ili kusafishwe mazingira na kuleta usuluhisho na muungano baina ya bibi na bwana.

Usuluhisho miongoni mwa watu

Imepokelewa kutoka kwa Mtume Muhammad s.a.w.w. akiwa amesema :

> *"Hakuna tendo lililo bora kabisa baada ya kutimiza yaliyo faradhishwa kama vile kuwasuluhisha watu ! Hii ni kheri ambayo inayoeneza kheri duniani kote."*

Al-Imam 'Ali ibn Abi Talib a.s. amesema kuwa Mtume Muhammad s.a.w.w. alisema wakati wa *usia, katika Wasa'il al-Shiah , Kitab Hajj, mlango 141* :

> *"Ewe Ali ! Bila shaka Allah swt anapendelea uwongo katika kusuluhisha na hapendezewi ukweli katika kuzua ufisadi na magomvi !"*

Vile vile Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema :

> *"Kusuluhisha miongoni mwa watu, kufikiria usulihisho na kuepusha magomvi ni bora kuliko sala na saumu."*

Abu hanifa Saiq Al-Hajj anasema kuwa kulizuka mgogoro baina yake na mume wa binti yake juu ya masuala ya mirathi. Wakati tukiwa tunazozana, alipita Wakili wa Al-Imam Ja'afar as- Sadiq a.s. aliyeitwa Mufadh-dhal ambaye alisimama hapo kwa muda na kuyasikia yote yaliyokuwa yakiendelea na kutuita nyumbani kwake na akatupa Dirhamu mia nne ambazo zilimaliza ugomvi baina yetu. Hapo ndipo aliposema :

> *"Hii mali ambayo mimi nimewapa si mali yangu bali ni mali ya Al-Imam Ja'afar as- Sadique a.s. Yeye ndiye amenipa amri kuwa pale wanapogombana masahaba wake, basi uwe ukimaliza magomvi yao kwa kutumia mali yangu…."*

Kwa hakika hapa ndipo tunapokuja kujua umuhimu wa suluhisho na upatanisho !

Mtume Muhammad s.a.w.w. alisema kuwa kazi hii ni afadhali kuliko hata sala na saumu. Ingawaje kazi hii ni *Sunnah* tu ambapo sala na saumu ni mambo yaliyo faradhi. Na sababu kubwa ni kwamba sala na saumu inaifanya nafsi ya mtu kuwa njema wakati ambapo kwa kusuluhisha na kupatanisha kunaufanya umma mzima uwe mwema na hivyo sala na saumu vitatimizwa katika mazingira mazuri. Waislamu wakiwa na ushirikiano na kupatana si vema kwa akhera tu bali hata maisha ya duniani pia yana faida kubwa. Wakati nyoyo za Waislamu zinapokuwa zimeungana basi kunaleta nguvu madhubuti ya umoja ambayo si udhahiri wake unaowakabili maadui tu bali inarahisisha kukabili adui wa ndani ya nafsi yaani Sheitani.

Maji ya Kur na umoja wa moyo

Umoja na maafikiano ya nyoyo za watu unaweza kutolewa kwa mfano wa maji ya *kur*[3] yaani iwapo kutakuwapo na vyombo vidogo vidogo vyenye maji yaliyo kasoro ya *kur* na kama yataingiwa na unajisi wowote hata kama kitakuwa kidogo, basi maji hayo yatakuwa najisi na si tohara tena lakini iwapo maji hayo hayo yaliyomo katika vyombo vidogo vidogo yatakapokusanywa katika sehemu moja ambapo yakafikia kiasi cha *kur* basi si kwamba hayatakuwa najisi pale

yatakapoingiwa na kitu kilicho najisi bali kitakuwa na uwezo wa kukitoharisha kwa urahisi sana kile kitakachokuwa najisi. Kwa hivyo zitakapokuwa nyoyo za Waislamu zimekuwa kitu kimoja basi baraka za Allah swt zitawafikia na Allah swt atawahurumia na kila faida za umoja wao utamfikia kila mmoja wao. Si hayo tu bali kwa kutokana na umoja wa nyoyo zao, Dini ya Uislamu itakuwa madhubuti maradufu. (umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu).

Vile vile kuna fadhila nyingi mno kwa ajili ya sala za jamaa' na zina thawabu nyingi. Kutendeana mema katika udugu wa kidini, kumsaidia na kuwa na uhusiano naye, haya mambo yanayo thawabu kubwa mno. Vile vile kushirikiana na kuungana na Mumin mwenzako na kupeana naye mikono na kubusu yanaleta thawabu kubwa mno. Kwa hakika kufanya usuluhisho miongoni mwa waumini wawili, thawabu zake hazina kifani na kufanya urafiki kwa ajili ya Allah swt ,kunapewa thawabu nyingi mno. Mambo haya kama yalivyo mambo mengine yanathawabu nyingi mno na hivyo tumeweza kutambua kuwa yote haya ni katika kuunganisha nyoyo za Waumini ziwe zimeungana bila ya kuwapo chuki na uadui wa ina yoyote miongoni mwao.

- Ama jambo la tatu, yaani kuwapatanisha na kuwaunganisha watu, Uislamu unataka kuwepo uhusiano wa kidugu na kirafiki miongoni mwa watu, na pale panapotokea mtafuruku baina yao au kati ya watu wawili, basi ni lazima kufanyike jitihada za kuwaunganisha na kuwapatanisha. Kwa hakika kuondolewa kwa tofauti baina yao ndiyo faida na maslahi ya jamii nzima kwa ujumla. Na hivyo, kusema uwongo kwa nia ya kuwapatanisha watu walio katika ugomvi kumeruhusiwa katika Uislamu.

Mtume Muhammad s.a.w.w. amesema :

"Hakuna uwongo kwa mtu anayesuluhisha."

Amesema al-Imam Ja'afar as- Sadiq a.s. :

"Uwongo ni uovu na haukubaliki isipokuwa katika sura mbili :

- *Katika kuuondoa shari ya mdhalimu*
- *Kuwapatanisha watu."*

Kwa kusema kwa ujumla, popote pale patakapokuwa na kusudi la kuondoa shari ya mdhalimu anayewasambaratisha Waislamu na kwa kuwasuluhisha watu, basi Uislamu unatambua kuwa uwongo katika sura hizi si dhambi tena. Hapa uwongo unaruhusiwa.

Kwa kukamilisha, ni lazima ikumbukwe kuwa 'uwongo mweupe' unavyojulikana unaruhusiwa katika sura ambazo Uislamu umeruhusu tu, ambapo katika sura nyingine itakuwa ni tendo la dhambi kutumia uwongo.

Hata hivyo uwongo unaotumiwa kwa kujipatia faida na kujipatia chochote kwa maslahi yake mwenyewe haviwezi kutambuliwa kama 'uwongo mweupe' na hivyo imeharamishwa katika Uislamu kwa mujibu wa Ayah za Qur'an Tukufu na hadithi za Mtume Muhammad s.a.w.w. na Maimamu a.s kutenda dhambi kutampatia adhabu kali huko akhera.

Uwongo vitani

Kwa mujibu wa riwaya ni kwamba iwapo itabidi kusema uwongo ili kuweza kuyashinda majeshi ya makafiri, basi katika sura hii unaruhusiwa.

- Ama kuhusiana na kudanganya vitani, wasomaji wetu mnajua kuwa Uislamu haupendelei vita na kile kinachomaanishwa hapa kwa vita ni baina ya haki na batili, ambavyo udanganyifu hapa utaimarisha haki na kuwadhoofisha batili, na hivyo inakubalika.

Kumuahidi mke wako

Mtume Muhammad s.a.w.w. anasema :

> *"Zipo nafasi tatu ambapo uwongo unapendeza: kudanganya katika vita, ahadi aitoayo mume kwa mke wake na kuwapatanisha watu."*

Maelezo:

- Ama kuhusiana na ahadi ya mume kwa mke wake, Uislamu unapendelea kuwaona wakiishi kwa raha na mustarehe waishi kwa kupendana. Hivyo kumwambia mke wako uwongo wa kumtimizia jambo fulani, kama unao uwezo basi vyema kabisa, lakini kama hana uwezo, basi anaweza kumpa ahadi ya uwongo ili kuepukana na ugomvi na kumuudhi mke wake.

  Kwa mfano, wewe hauna uwezo wa kumtimizia ombi fulani la mke wako, kama kwa mfano anataka nyumba, lakini wewe kwa kutokuwa na uwezo huo, utamdanganya kuwa nitakujengea au kukununulia ili kumridhisha mke wako. Sote tunajua kuwa *ukaidi wa mwanamke ni ukaidi mkubwa kabisa* na vile vile Al-Imam ‘Ali ibn Abi Talib a.s. amesema kuwa “mwanamke ni kama mfupa wa ubavu, upo umepinda, hivyo usijaribu kuunyosha, utavunjika” hivyo tutumie mbinu kama hizi kwa nia njema ili kutuliza mambo nyumbani.

Mume anaweza kumpa ahadi mke wake pale atakapokitaka kitu hicho mke wake, basi yeye yeye atoe ahadi kuwa atamtimizia ingawaje yeye hana nia wala makusudio ya kumtimizia.

Lakini kuruhusiwa huku kwa ahadi za namna hii ni mushkeli. Ingawaje zipo riwaya dhaifu zinazozungumzia kuruhusiwa kwa ahadi kama hizo.

Lakini iwapo mtu anajua kuwa endapo yeye hatampa ahadi za uwongo mke wake, basi kutazuka ugomvi na vita vikali nyumbani mwao au mke wake atamkasirikia na kununa sana au kuna hofu ya kupeana talaqa basi katika sura kama hizi zisizo na njia nyengine, anaruhusiwa kutoa ahadi za uwongo.

Hofu ya adhabu na matendo mema

Al-Imam ‘Ali ibn Abi Talib a.s. amesema katika *Al-Kafi (ikizungumzia thawabu za Allah swt na juu ya adhabu na matumaini ya kusamehewa)* :

> *“Jiepusheni na kusema uwongo ! Pale mtu anapotarajia kupata kitu basi anataka akipate tu hicho kitu (basi huwa tayari kufanya kazi yeyote ili aipate) na vile vile mtu anapo kiogopa kitu chochote kile, basi hujiweka mbali nacho.”*

Hapa Al-Imam ‘Ali ibn Abi Talib a.s. anaeleza wazi kuwa mtu anapotaka kujichumia thawabu na anakuwa na mategemeo ya thawabu hizo basi kamwe hatakiwi kusema uwongo lakini mategemeo haya ni kule kufanya matendo mema. Kusema uwongo ni tendo lililoharamishwa na ni jambo baya na ovu sana na kwa hakika iwapo mtu anaziogopa adhabu za Allah swt basi inambidi ajitayarishe kuyakimbia madhambi kwa sababu kutenda madhambi kunamfanya mtu awe mustahili wa adhabu kali za Allah swt .

Iwapo kutakuwepo mtu ambaye anadai kwa mdomo tu kuwa yeye anategemea thawabu kutoka kwa Allah swt na anaziogopa adhabu zake na ilhali haachani na madhambi na wala hatendi matendo mema, basi mtu kama huyu ni **mwongo** na anajidanganya mwenyewe.

> Al-Imam ‘Ali ibn Abi Talib a.s. amesema katika *Nahjul-Balagha,* :“Mtu yeyote anayefikiria kuwa yeye anamtegemea Allah swt lakini matendo yake hayaonyeshi hivyo basi kwa kiapo cha Allah swt aliye Mkuu, mtu huyo ni muongo. Ingawaje mtu anapo kitegemea kitu basi mwenendo wake hudhihirisha hivyo. Lakini itawezekanaje yeye amtegemee Allah swt ambapo matendo yake hayadhihiri hivyo ? (mtu kama huyu kwa hakika si miongoni mwa wale wanao mtegemea Allah swt basi anajidanganya mwenyewe). Vile vile mtu anapo kiogopa kitu chochote basi matendo yake yatadhihirisha hali hiyo yaani ataamua kukikimbia kitu hicho. Lakini mtu anapodai

kuwa anamwogopa Allah swt ni kwa nini sasa hakimbii mbali na madhambi ?"

Iwapo mtu atakuwa akidai kumtegemea Allah swt na kuwa na khofu ya Allah swt ambapo matendo yake hayatoi uthibitisho huo, basi huyo ni mwongo kama vile mtu anavyodai kuwa na sifa za subira, shukurani, kukubalia, uchamungu lakini haoneshi hivyo kimatendo, basi naye pia ni mwongo !

Kile kilicho mdomoni ndicho hicho hicho kiwe moyoni

Al-Imam Ja'afar as- Sadique a.s. amesema katika *Misbah As-Shari'ah* :

"Wakati msemapo Allahu Akbar, basi muelewe kile kilicho baina ya mbingu za juu na ardhi, vyote ni vidogo mbele ya Allah swt na kwa undani wa moyoni mwenu muelewe kwa sababu Allah swt anapoona kuwa kuna mja wake ambaye hasemi Allahu Akbar kutokea undani mwa moyo wake, basi Allah swt (humwambia) 'Ewe mwongo ! Wewe unataka kunidanganya basi kwa kiapo cha heshima na Utukufu Wangu basi mimi nitakuepusha na dhikr yangu !'"

Kwa masikitiko makubwa sana kuna baadhi ya watu ambao ingawaje kwa mdomo wanatamka *Allahu Akbar* lakini matendo yao na mioyoni mwao wanadhihirisha kuwa *Allahu Asghar* (Allah swt atuepushe na dhambi kama hili) (yaani Allah mdogo). Yaani watu kama hawa ukiwaambia wafanye jambo fulani kwa ajili ya Allah swt au wasifanye jambo fulani kwa ajili ya Allah swt , basi wao hawatajali chochote ! Lakini iwapo utawapa mapesa kidogo basi watakubali maneno yako papo hapo. ! Yaani mapesa ndiyo makubwa machoni mwao, na wala si Allah swt ambaye ndiye mkubwa (Allah swt atuepushe nayo) ! Vile vile wapo watu wanaoamini kuwa iwapo wao hawatafanya kazi njema fulani au kama hawataacha kufanya jambo fulani baya basi watapatwa na matatizo na majanga au kuna mtu atakayewasumbua. Kwa sababu hizo basi utamwona huyo mtu anatekeleza maamrisho hayo ama ya kutenda au kuacha. Lakini iwapo mambo hayo yangalikuwa yatekelezwe kwa ajili ya Allah swt tu, basi kamwe asingalifanya hivyo !

Kufanya ‘ibada na uwongo

Iwapo mtu atakuwa akifanya ibada ya Allah swt na akasema “*Sisi tunafanya ‘ibada yako tu na tunakuomba Wewe tu msaada….”* na kumbe usiku na mchana akawa anaabudu mapesa na mali na yupo katika kushibisha tumbo lake na kutimiza matamanio yake, na wala hana lingine katika maisha yake, sasa je mtu kama huyu unaweza kusema kuwa ni mkweli ?

Je kwa kweli mtu kama huyu ni mfanya ibada ya Allah swt ? Iwapo mtu atategemea sababu zilizodhahiri tu na kuziamini, na akaviomba msaada hivyo tu, jee mtu kama huyu tutaweza kumwita mkweli ?

Kwa kusema *Iyyaka na’abudu wa Iyyaka Nasta’in* na iwapo tutaka ya khilafu, basi huo pia ni uwongo.

Uwongo katika Dua

Sisi huwa tunadai uwongo katika Dua tuzisomazo ! Mfano, iwapo mtu atasoma na kusema *Radhitu billahi Rabban* yaani mimi nipo radhi na Allah swt na ninayo furaha naye kwa kuwa Yeye ndiye anayenilea … Yeye ndiye mwenye kulea viumbe vyote na mimi nipo radhi nae.
Sasa iwapo mtu hatakuwa radhi kwa kile alichopewa na Allah swt kwa *Qadhaa wa Qadr* (hiari na ushurtisho). Yaani iwapo kutatokea jambo lililo kinyume na vile alivyokuwa akitaka na kutarajia, basi huwa mwepesi kumkasirikia Allah swt na huanza kutoa mashitaka dhidi ya Allah swt ! Mashitaka hayo ndiyo uthibitisho kuwa huyo mtu ni mwongo !

Kukiri kuwakubali ‘Aimma a.s. na kusema uwongo

Mtu anaposema kuwa :*”Mimi ninayo furaha kuwa Mtume Muhammad s.a.w.w. ni Mtume wangu na Qur’an Tukufu ni kitabu Kitakatifu na kuwa Al-Imam ‘Ali ibn Abi Talib a.s. ni Imamu wangu. Na vyote hivyo vipo kwa ajili ya kuniongoza.”* Ingawaje anatamka kwa mdomo lakini kimatendo utaona kuwa Shetani na matamanio yake ya *nafsi* ndio

viongozi wake ! Na huvifuata hivyo ! Utaona kuwa yeye hatilii maanani mafunzo na hidaya ya Qur'an Tukufu . Na vile vile hatilii maanani maamrisho na mafunzo yaliyotolewa na Maimamu a.s. Kwa hivyo mtu kama huyu ni mwongo.

Je anasema kweli ?

Wakati mtu anapofanya dua na akasema *"(Ewe Mola wangu !) Mimi ninapoziangalia dhambi zangu basi hulia na ninapoangalia ukarimu wako ninajawa na matumaini kuwa Wewe utanisamehea."* Kwa hakika utaona kuwa tunatamka hivyo lakini hatujali madhambi na hata anapotambua kuwa jambo fulani ni dhambi, basi hulitenda bila ya woga wowote ule ! Uso wake haushtuki hata punje kidogo wakati wa kutenda dhambi ! Basi hujitoa katika ukarimu na rehema za Allah swt ! Je mtu kama huyu anapoyatamka maneno kama hayo yalivyo katika dua, anasema ukweli ? Je uwongo wake si upo wazi !?

Vile vile mtu anapotamka *"Mimi ninalia kwa kutokwa nafsi yangu na ninalilia maswala ya kaburini na ninalilia khofu ya Qiyama"* ingawaje ni dhahiri kuwa hakuna kitu kama hicho anachokililia. Huo ni uwongo wake kwani matendo yake hayaonyeshi kama kweli anayo khofu kama hiyo moyoni mwake. Al-Imam Zaynul 'Aabediin a.s. amesema katika *Dua-i-Abu Hamza Thumali* : "*Ewe Allah swt ! Labda Wewe umenipata katika ngazi za waongo na kwa hivyo (umeniondolea mtazamo wako wa kirehema) na umeniacha katika hali niliyonayo."* Yaani mimi nimekuwa nikiyatimiza matamanio ya nafsi yangu na wala sijui nitaangukia katika maangamizo yapi.

Kuwaambia uwongo Maimamu (a.s.)

Mfano wa kuwaambia uwongo Maimamu a.s. ni kama vile tunavyosema katika *Ziyarat* : *"Enyi Aimma Ma'asumiin a.s.! Mimi nimezikubali kauli zenu na ninafuata hukumu (na maamrisho) yenu na mimi ni mwenye kuwatiini."* Sasa iwapo mtu atazisikia kauli na maamrisho ya Maimamu a.s. na asizifuate na badala yake akafuata

matamanio na amri ya nafsi yake basi mtu kama huyu ni shetani ! pia inadhihirika waziwazi kuwa huyo ni muongo kwa Maimamu a.s. !

Vile vile mfano mwingine wa kusema uwongo upo unapatikana katika Ziyarat, wakati tusemapo :*"Enyi Aimma watoharifu ! Mtu yeyote aliye na amani pamoja nanyi basi mimi pia nitakuwa na amani pamoja naye na yeyote yule atakayepigana vita pamoja nanyi au kuwapinga basi nami nitakuwa na vita naye na nitampinga vile vile !"* Kwa hakika hivyo ndivyo tunavyodai, lakini matendo yetu ni kwamba tunao urafiki mzuri wa kidugu pamoja na maadui wa Uislamu ! Na tunafanya uadui pamoja na wapenzi na wafuasi wa Aimma a.s.. Wakati anaposema *"Enyi Maasumiin a.s. ! Mimi ninawaacha wale wanaokukhilafu ninyi."* Lakini kwa hakika haya hayatekelezwi kimatendo Sasa jee mtu kama huyu si muongo mbele ya Maimamu a.s. ?

Sasa je tuombeje Dua ?

Iwapo inaonekana kuwa mtu anapomuomba Allah swt na kusoma Ziyarat kwa ajili ya Mtume Muhammad s.a.w.w. na Maimamu a.s. huku anajua kuwa yeye ni mwongo, sasa jee afanyaje Dua au Ziyarat ?

Kwa hakika hatutaweza kulijibu swali hili kwa undani zaidi kwani kitabu hiki hakiandikwi kwa maudhui haya, hata hivyo tutawaleteeni machache kwa kuwaelezea kwamba, uwongo tuliofanyia ishara hapo juu, ni kutaka kujiepusha na *'ujb, kujipenda, umaghururi n.k.*. Isije ikatokea kuwa Mumiin akajifakharisha kwa Dua na dhikri za Allah swt . Na hali hii kamwe isije ikatokea.

Iwapo mtu atasema kuwa kwa kuwa sisi hatusemi ukweli katika Dhikri za Allah swt na Dua' na Ziyarat, basi tuviache. Kwa hakika mawazo potofu kama haya ni mawazo na fitina za kishetani. Tutambue waziwazi kuwa shetani anataka mtu huyo asipate thawabu za kufanya Dhikiri na kusoma Dua' na hivyo mtu huyo hatabarikiwa. Kwa hakika si kila mtu huwa mkweli kuanzia mwanzoni, isipokuwa ni matunda ya jitihada na mioyo yetu ya kuelekea katika ukweli ndio inaotufanya sisi kuwa wakweli. Na bila shaka katika vuguvugu letu la harakati hizo hazikosi baraka za Allah swt ambazo zitatufikisha katika malengo yetu.

Maneno yanayozungumwa katika Du'a ama mtu anaelewa maana yao au haelewi. Basi iwapo atakuwa akielewa maana zake, basi moyo wake utakuwa unafurahi kwa kuyaelewa yale anayoyasoma na hivyo hakosi baraka na rehema za Allah swt na Mtume Muhammad s.a.w.w. na Maimamu a.s. Ama kwa mtu asiyeelewa maana zake hatuwezi kusema kuwa ni mwongo. Lakini inabidi sisi tujitahidi kiasi tuwezacho katika kuelewa maana ya yale tuyasomayo, na si kwamba tusome tu, ni lazima tufaidike kwa maana na baraka zake.

Kila mtu ana daraja lake

Lakini wale ambao wanasoma Qur'an Tukufu na Du'a na kuyaelewa maana yake inawabidi kujua kuna daraja mbalimbali. Daraja lililo la juu kabisa ni la Ma'asumiin a.s. ambao ndio wenye upeo wa juu kabisa katika kuyajua na kuyafuata kwani wao ndio watoharifu na wauminii kwao si rahisi kufikia ngazi hii. Sasa tutawezaje kusema kuwa wao wanasema uwongo ?

Hivyo sisi tunaweza kusema kuwa waumiin hawasemi uwongo. Mfano kwamba kila Mumiin anakuwa na khofu ya Allah swt kama vile tunavyoambiwa katika Qur'an Tukufu : *'Kama nyinyi ni waumiin wa kweli basi muwe mukiniogopa Mimi tu'* (Surah Aali-Imran, 3, Ayah ya 175) Na vivyo hivyo waumiin wote ndio wanaomtegemea Allah swt tu na bila shaka wote wanakuwa na khofu ya Allah swt na matumaini yao pia yanakuwa na ngazi mbalimbali na kamwe haiwezekani zikalingana na za Aimma a.s.

Kwa kuwa Mumiin hushawishiwa na matamanio ya nafsi yake na kwa kuwa hawakufikia utukufu wa utakasisho wa nafsi zao, basi huwa rahisi kutumbukia katika madhambi na hivyo hutokea dosari na kasoro katika ufuatiliaji na utekelezaji wa maamrisho ya Allah swt. Kama vile tunasoma katika Dua-i Abu Hamza Thumali :*"Ewe Allah swt ! Mimi madhambi niliyoyatenda si kwamba nikukupinga wewe na wala sikutenda madhambi hayo kuwa nikichukulia hukumu zako ati ni za kawaida na wala sikutenda madhambi kwa kufikiria kuwa adhabu zako ni ndogo bali nimetenda kwa kutokana na kasoro zangu za kinafsi na ujeuri wangu.."*

Yakini na uhalifu

Mtu pamoja na kuwa na imani na yakini katika adhabu ya Allah swt, na kuyajua hayo pia utaona kuwa bado anatenda madhambi na hii ni kwa sababu ya kughilibiwa na matamanio ya nafsi yake. Hii si lazima kuwa mtu anapokuwa na yakini ya Allah swt asitende madhambi. Watu wengi wanadai kuwa watu waliokufahawanatofauti kwa sababu mfu hauwezi kufanya harakati zozote wala hakuna kazi inayoweza kufanywa nao. Lakini pamoja na kuwa na yakini ya hayo bado anaogopa usiku kubakia peke yake pamoja na maiti katika chumba kimoja na hujawa khofu. Na kwa hakika hii ndiyo sababu tunasoma katika Du'a :*"Ewe Allah swt ! Nakuomba unipatie yakini ya kweli kwayo ambayo mimi niweze kutii amri zako kikamilifu."*

Iwapo mtu kwa hakika atamwomba Allah swt amjaalie khofu ya kweli moyoni mwake, basi Allah swt atamfanyia hivyo na kumsamehe madhambi yake, na itakaa inaongezeka ngazi katika khofu yake kama vile ngazi ya utiifu na ibada inavyoongezeka vile mtu afanyavyo jitihada zaidi na zaidi.

Inapatikana katika riwaya kuwa *"Mtu anapokitaka kitu basi kwa kufanya jitihada, anakipata tu."*

Kwa hakika tunaona kwamba'ukweli' unawapendeza Ma'sumiin a.s. tu na ndiyo maana hii tunaambiwa katika Qur'an Tukufu katika Surah at-Tawbah, 9, Ayah ya 119 : *'Muwe pamoja na Wasemao ukweli.'* Katika Ayah hii Allah swt anatuambia kuhusu 'Sadiqiin' ambao ndio Ahlul Bait a.s. ya Mtume Muhammad s.a.w.w. .

T A M A T I
WALHAMDU - LILLAH

1. Hiki kitabu ni juzuu ya pili katika maudhui haya na kwa kuliona suala hili ni nyeti katika jamii yetu, ndiyo maana nimekitayarisha hiki kitabu cha juzuu ya pili

*[2]. Msomaji unashauriwa kukisoma kitabu nilichokitarjumu kiitwacho '**Tadhwin al-Hadith** yaani **Historia ya ukusanyaji na Uandishi wa Hadith**. Kwa hakika utafaidika mno iwapo utakisoma. Au unaweza kukipata katika Internet : http://www.al-islam.org/kiswahili*

[3] Kur yaani yenye ujazo wa maji ya 27 za mraba wa shibiri za ujazo (3x3x3).

` Ni vyema kutengeneza 42 7/8 mraba shibiri (3 ″ X 3 ″ X 3 ″) (1 shibiri = 9 inchi)